GAZETI LA KWANZA LA ISLAM KUTOLEWA KWA LUGHA YA KISWAHILI - MWAKA 1936

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA

Mapenzi Yamungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

JUZU NO. 237 **Al Ula-Al Akhirah** 1445 **AH** **DISEMBA–** 2023 **ZAHOOR** 1402 **HS** **BEI TSH 800/=**

>UK .5 **Yesu aliongozwa na nani Nyikani?**

Imani na Dhabihu ya Kifedha

Uzinduzi wa Mwaka wa Tahrik Jadid 2023.

'Kutumia Kati ya Kile Unachokipenda - Kiini cha Tahrik-e-Jadid'.

Baada ya kusoma Tashahhud, Ta'awwuz na Surah al-Fatihah, Mtukufu, Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[atba] alisoma aya

UK. 10



Hadhrat Ameerul Mumineen Mirza Masroor Ahmad Khalifatul Masih wa tano[atba] akihutubia waumini katika Msikiti wa Baitul Futuh, Morden, London, Uingereza – Siku ya tarehe 03 Novemba 2023, juu ya kujitolea katika Kifedha.

Mwaka Mpya kutangazwa Tahrik Jadid

Tanzania namba 4 Afrika

Majlis Khuddamul Ahmadiyya Dar Yafanya Darsa la malezi kwa Khuddam & Atfal.

Na: Isihaka Nyamihasi,
Dar es Salaam.

Tanzimu ya khuddamul Ahmadiyya na Atfal Mkoa wa Dar es salaam kwa kushirikiana na Sadri majlis Khuddam Taifa,Bw. Rahim Mwanga Sahib na Qaid wa mkoa Bw. Said Ponela Sahib amefanikiwa kufanya darsa la malezi (Tarbiyyat Class) kwa khuddam na Atfal wa mkoa wa Dar es Salaam siku ya jumapili ya tarehe



12 November 2023, Masjid salaam Mnazi mmoja. Miongoni mwa malengo makuu ya darsa hilo ni kuinua na kukuza Imani za wanatanzimu,kwa kuyafata mafundisho sahihi ya Islam na Jamaat Ahmadiyya kama yalivyo maelekezo ya Kharifa mtukufu v (a.t.b.a) juu ya kufanya Tarbiyyat kwa wanajamaat wote.

Zoezi hilo lilianza asubuhi ya saa 08:30, Baada ya Sadri Majlis Khuddam kuongoza Maombi ya ufunguzi kisha usomaji wa Qur'an tukufu na Shairi uliosomwa na Mwl Mohammed Habibu,na baadaye Qaid Sahib akaongoza kiapo cha Khuddam

Kuiendea Elimu na matumizi yake yenye Baraka kwa mujibu wa.. UK. 8

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Bila utafiti huna haki.

Wasomi wamejiwekea kanuni hapo juu. Ni kanuni nzito na inatakiwa kuheshimiwa na kila msomi anayejiheshimu na kuheshimu taaluma yake.

Inasikitisha kuona ya kwamba wasomi wa Magharibi kwa sababu ya husuda na chuki iliyopitiliza wameimwagia Islam lawama pamoja na Mtukufu Mtume Muhammad[saw] kwamba kwa upanga watu walilazimishwa kuingia katika Islam. Wapo wasomi wengi waliofanya hivyo, lakini leo tutamtizama Profesa mashuhuri wa Marekani John William Draper ambaye ameandika vitabu na kilichompa umaarufu ni ***History of the Conflicts between Religion and Science***. Kwenye ukurasa wa 67 wa kitabu hicho anaandika kuhusu Mtukufu Mtume Muhammad[saw].

He extinguished idolatry in Arabic by force and prepare to make War on the Roman empire - Aliteketeza kuabudu masanamu. Uarabuni na kujitayarisha kuingia vita na Roma. Kauli isiyo hata chembe ya ushahidi wa kihisitoria.

Uhuru wa kusema upo. Uhuru wa kuandika nao pia unaheshimiwa. Lakini kinachoheshimiwa zaidi ni wale wanao kusikiliza, uwaheshimu na ujenge hoja. Bila ushahidi hizo zinakuwa ni porojo za Bi. Kizee akiwafurahisha wajukuu zake wakati wanachoma mahindi usiku.

Mafundisho ya Islam yako wazi na maisha ya mtekelezaji wa mafundisho hayo ni kitabu kilichowazi. Ushahidi wa kutosha unatangaza kuwa hakuna karaha katika Dini. Na upo uhuru wa kuchagua - Shakira ima Kafura. Katika Kuruani Tukufu Al-Kahf 18:20 Allah anasema: Wasema: ukweli umetoka kwa Mola basi anayependa akubali na asiyependa akatae. Dhana hiyo pia inaelezwa Sura Yunus 10:109. Sema enyi watu haki imekwisha wafikieni toka kwa Mola wenu basi anayeongoka kwa faida ya nafsi yake. Sura Al Baqara 2: 257 hakuna karaha katika Dini. Huo wote ni ushahidi kuwa kinachotakiwa ni kutumia akili kukubali au kukataa.

Maisha ya Mtukufu Mtume Muhammad[saw] hayakuwa chochote, isipokuwa kama alivyosema Mama wa waaminio Bi Aisha[ra] ***Kurani***. Kila hatua ya maisha yake Mtume wa Allah[saw] alitekeleza mafundisho ya Kuruani Tukufu. Hakuna mfano hata mmoja wa kuonesha kuwa Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alilazimisha mtu yeyote kuingia katika Islam. Balozi fulani alitumwa kwa Mtukufu Mtume Muhammad[saw] na baada ya mazungumzo aliathirika sana na kutaka kujiunga na Islam. Alimuambia kwanza atekeleze kazi aliyopewa na kama ameona haki basi afunge safari ya kuja kujiunga na Islam. Hata aliyetoa shahada na akauwawa kwa sababu alifikiriwa ametamka shahada hiyo kwa hofu. Tendo hilo lilimkasilisha sana Mtume[saw] na kumuuliza aliyehusika, je uliingia katika roho yake?

Ingawaje tumesema hakuna hata mmoja aliyelazimishwa katika Islam bado tunasema kwa unyenyekevu kuwa si kweli kwamba tunajua yote. Tuko tayari kujifunza. Tuko tayari kumpokea huyo aliyeingizwa katika Islam kwa nguvu, kwani kama anvyosema mwandishi wa ***War and Peace by Leo Tolstoy,*** *kile tu ambacho tunajua ni kwamba hakuna tunachokijua. Na hicho ndio kilele cha hekima ya binadamu*.

Kama tulivyosema hapo mwanzo kuwa ni muhimu kufanya utafiti kabla hujasema. utafiti huo utakusaidia kuonesha kwamba Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alikuwa na shauku kubwa ya mapatano na amani. Alipofika Madina jambo la kwanza alilolifanya ni kuwekeana mkataba na Wayahudi. Mkataba wa amani. Makubaliano ya Hudaibiya kwa jicho la kawaida lilikuwa ni tukio la udhalilishaji na kushindwa kwa Islam. Mtukufu Mtume Muhammad[saw] alikubali masharti aliyopewa kiasi hiki ya kwamba Islam ikaonekana imeonewa sana. Lakini Allah akatangaza kuwa huo ulikuwa ni Ushindi mkubwa. Historia inaonesha kuwa mara baada ya mkataba huo palikuwa na kipindi kirefu cha amani. Wakati huo kuliko wakati mwingine wowote. Islam ilipanuka na mahubiri makubwa kufanyika. Ni wakati wa amani Islam ilipopata wafuasi wengi. Wanasemaje wanaotoa masingizio kuwa Islam ilienezwa kwa Upanga? Someni kwa utulivu hisitoria ya Islam bila Miwani ya rangi na bila shaka mtagundua kuwa Islam ilienezwa kwa hekima na mawaidha mema na mvuto mkali kuliko sumaku wa Mtukufu Mtume Muhammad[saw] ambapo kijana mtumwa alikataa kuongozana na wazazi wake baada ya kupata uhuru na akasema nawezaje kuwa mbali na Mtukufu Mtume Muhammad[saw]? Mvuto huo wa Mtukufu Mtume Muhammad[saw] umethibitisha kauli ya Allah "Kwa hakika una Hulka Njema».




QUR'AN TUKUFU

22. SURA AL-HAJJ

ذٰلِكَ ۚ وَمَنْ يُّعَظِّمْ حُرُمٰتِ اللّٰهِ فَهُوَ خَيْرٌ لَّهٗ عِنْدَ رَبِّهٖ ؕ وَ اُحِلَّتْ لَكُمُ الْاَنْعَامُ اِلَّا مَا يُتْلٰى عَلَيْكُمْ فَاجْتَنِبُوا الرِّجْسَ مِنَ الْاَوْثَانِ وَاجْتَنِبُوْا قَوْلَ الزُّوْرِ ۙ﴿۳۱﴾


31. Ndivyo hivyo; na anayevitukuza vitu vitakatifu vya Mwenyezi Mungu, basi hiyo ni heri kwake mbele ya Mola wake. Na mmehalalishiwa wanyama isipokuwa wale mnaosomewa; basi jiepusheni na uchafu wa masanamu na jiepusheni na usemi wa uwongo.



NUKUU YA HADITHI

عَنِ ابْنِ عُمَرَ ، عَنِ النَّبِيِّ صَلَّى اللَّهُ عَلَيْهِ وَسَلَّمَ أَنَّهُ نَهَى أَنْ يُقَامَ الرَّجُلُ مِنْ مَجْلِسِهِ وَيَجْلِسَ فِيهِ آخَرُ ، وَلَكِنْ تَفَسَّحُوا وَتَوَسَّعُوا ، وَكَانَ ابْنُ عُمَرَ يَكْرَهُ أَنْ يَقُومَ الرَّجُلُ مِنْ مَجْلِسِهِ ، ثُمَّ يَجْلِسَ مَكَانَهُ .

(Sahih Bukhari, HADITH NO:6270) imesimuliwa na Ibne Omar r.a. kwamba Mtume saw alikataza kuwa, mtu aondolewe kutoka katika mahala pake na ake mwingine humo ila muwe na wasaa na kuapa nafasi wengine(kwa ajili ya kukaa) na Ibne Omar r.a.alikuwa hapendi kwamba mtu atoke kutoka mahala pake ili yeye ake humo.



Nukuu ya Masih Aliyeahidiwa[as]

KUMBUKA AKHERA ==========

na ni jambo hili ambalo ni kweli kwa maisha. Kumbuka kwamba hali za maisha ya mtu ziko katika kumjua Mungu Mwenyezi. Nani anajua maisha yamewaandalia nini? Ndiyo maana ni lazima mtu mmoja-mmoja auamshe moyo wake daima ili kuufanya uwe macho. Inasikitisha kuwa japo madhila yameenea lakini jeuri na kiburi kinachowala watu hakijapungua. Nasema kweli hazitafutiliwa mbali hadi ukaidi na chuki za wananchi ziondolewe. Ninaona kwamba watu hawajajitayarisha kikamili kupatanishwa na Mungu Mwenyezi. Katika kipindi cha njaa, watu walibaki bila kutikiswa. Katika nyakati za awali, amri ya kidini iliyotolewa kutoka Makka au Madina ingewatisha watu. Wakati mtu angesema kwamba amri imetolewa kutoka Makka, watu wangekuwa na kicho, lakini sasa hata maafa ya siku hizi hayawatie moyo hata kidogo. Ni rai yangu kwamba mpaka watu waelekee kwa Mungu kikamilifu, amri ya Mwenyezi Mungu haitabadilika kamwe. Mwenyezi Mungu Mtukufu anasema: اِنَّ اللّٰهَ لَا يُغَيِّرُ مَا بِقَوْمٍ حَتّٰى يُغَيِّرُوْا مَا بِاَنْفُسِهِمْ Hakika Mwenyezi Mungu habadili yaliyomo kwa watu mpaka wabadili yaliyomo nyoyoni mwao. *(Malfuzat Vol 1 uk 173-174) ====

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Dr. Swaleh Kitabu Pazi
Kompyuta: Jabiri Faraji Bishazo.
Mchapishaji: Sheikh Raghib Zia ul Haq
Msambazaji: Mwl. Omari Ali Mnungu
Wajumbe: 1. Mwl. Abdullah Khamis Mbanga
2. Mahmood Hamsin Mubiru.
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed, S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu36@gmail.com

Imani na Dhabihu ya Kifedha: Uzinduzi wa Mwaka wa Tahrik Jadid

Kutoka Uk wa 1..

ifuatayo, ambayo tafsiri yake ni:

'Hamtaweza kuufikia wema hasa mpaka mtoe katika vile mnavyovipenda na chochote mtakachokitoa, basi hakika Allah Anakijua. (Qur'ani Tukufu, 3:93)

Khalifa mtukufu (atba) amesema kuwa katika Aya hii, Mwenyezi Mungu amebainisha kwamba viwango vya juu kabisa vya wema hupatikana pale mtu anapotumia katika mali na vitu anavyovipenda.

Kutumia Kutoka Mali Uipendayo Hupelekea kwenye Wema wa Kweli

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alimnukuu Masihi Aliyeahidiwa (as) ambaye alisema kwamba wema wa kweli, ambao unaongoza kwenye wokovu, unaweza kupatikana wakati mtu anapotumia kutoka mali yake ya thamani na inayopendwa zaidi naye. Kutumia kutoka mali isiyo na maana hakuna maana, badala yake, mali ambayo ni ya thamani zaidi kwa mtu lazima itumike ili kuwa mpendwa zaidi kwa Mungu. Inawezekanaje mtu kufikia vyeo vya juu bila kustahimili shida? Maswahaba wa Mtukufu Mtume (saw) hawakutokea tu kupata daraja zao, bali walifikia hapo tu baada ya mapambano mengi. Wamebarikiwa wale wasiojali kustahimili matatizo kwa ajili ya Mwenyezi Mungu.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba hii ndiyo roho ambayo Masihi Aliyeahidiwa (as) alitaka kuitia ndani ya Jumuiya yake. Sasa, kuna idadi kubwa ya watu katika Jumuiya hii ambao huweka mahitaji yao wenyewe kando na badala yake kujitolea kifedha kwa ajili ya imani yao. Siku hizi, tunaona matatizo ya kifedha yakiongezeka duniani, hasa katika nchi zilizoendelea. Vita vya sasa duniani na uzembe wa wanasiasa umesababisha hali hii. Hata hivyo, pamoja na haya, dhabihu za kifedha za Waahmadiyya zimeendelea kuongezeka. Hili linaweza kuwa gumu kwa mtu wa kidunia kulielewa, lakini mtu wa imani anajua kwamba ni matokeo ya dhabihu hizo kwamba baraka za Mwenyezi Mungu huongezeka.

Matukio Ya Kuchochea Imani Ya Kujitolea Kuelekea Tahrik-e-Jadid

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba kama ilivyo desturi, Hotuba ya kwanza ya mwezi wa Novemba huwa inazindua mwaka mpya wa Tahrik-e-Jadid. Huzur Aqdas (atba) alisema kwamba atawasilisha baadhi ya matukio kuhusiana na Tahrik-e-Jadid.

Huzur Aqdas (atba) alisema kwamba amepokea orodha ndefu ya wanawake ambao wametoa dhabihu vito vyao vya dhahabu na kuvitoa kwa ajili ya Tahrik-e-Jadid. Moja ya majukumu ya awali ya Khalifa wa Pili (ra) mwanzoni mwa Tahrik-e-Jadid ilikuwa kwamba badala ya kutengeneza vito, wanawake wanapaswa kutoa utajiri huo katika dhabihu za kifedha. Hata hivyo, inaweza kuwa vigumu zaidi kuwa na kitu tayari katika milki yako na kisha kukitoa kwa njia ya dhabihu ya kifedha. Mifano kama hiyo inapatikana ulimwenguni kote.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba kuna mifano pia ya wale ambao hali zao za kiuchumi sio nzuri, lakini bado wanatoa dhabihu za kifedha, ambapo Mwenyezi Mungu huwapa neema Zake juu yao kwa njia zinazowafanya washangae. Wale ambao ni matajiri wanapaswa kujifunza kutokana na hili. Kuna mifano ya wale ambao hali zao za kiuchumi ni duni lakini hutoa asilimia hamsini au hata asilimia mia moja ya kile wanachomiliki kama dhabihu ya kifedha, ambapo baadhi ya watu matajiri wanatoa asilimia moja tu.

Huzur Aqdas (atba) alisema kwamba fundi pikipiki kutoka Guinea-Bissau alikumbushwa kutoa kitu kwa ajili ya Tahrik-e-Jadid na alitoa chote alichokuwa nacho mfukoni. Wakati huo huo, binti-mkwe wake alikuja kumwomba pesa za kuandaa chakula cha jioni. Kwa vile tayari alikuwa ametoa ahadi yake kiasi chote kwa ajili ya Tahrik-e-Jadid, alimwambia abaki mvumilivu. Muda usio mrefu akapigiwa simu na ofisi ya serikali ikisema kwamba muda fulani uliopita alikuwa akifanya kazi ya kutengeneza pikipiki zao lakini hakuwa amelipwa, na hivyo anapaswa kuja ofisini kuchukua hundi. Kwa njia hii, alibarikiwa mara moja kwa ajili ya dhabihu yake, na akaenda nyumbani na kuiambia familia yake kwa furaha juu ya kile kilichotokea.

Khalifa mtukufu (atba) alisema kuwa kuna mtu mmoja nchini Tanzania alifahamishwa na kampuni aliyofanyia kazi kuwa kutakuwa na kupunguzwa kwa mishahara kwa wafanyakazi wote. Ilikuwa ni wakati huo ambapo pia alipokea simu kuhusu kujitolea kifedha kwa ajili ya Tahrik-e-Jadid. Hakuonyesha wasiwasi wake kutokana na hali yake ya kifedha, na badala yake alilipa ahadi yake kikamilifu. Siku iliyofuata, alifahamishwa na kampuni yake kwamba ingawa mshahara wa wafanyikazi wengine ungekatwa, hakutakuwa na kupunguzwa kwa mshahara wake. Alihusisha hili na ukweli kwamba alikuwa ametoa dhabihu ya kifedha kwa ajili ya Tahrik-e-Jadid.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba kulikuwa na kijana huko Australia ambaye hakuwa ametoa michango yoyote ya kifedha kwa miaka kumi. Baada ya kuketi na mbashiri, alianza kutoa michango ya kifedha tena, ikijumuisha mchango wa Tahrik-e-Jadid. Muda fulani baadaye, alimpigia simu mbashiri huyo kumwarifu kwamba alikuwa amepandishwa cheo kazini jambo ambalo halikutarajiwa kabisa. Alihusisha jambo hilo na ukweli kwamba alianza kujinyima fedha, ambayo aliapa kwamba hataacha kufanya hivyo tena.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba huko Kazakhstan, mtu mmoja ambaye alikuwa akitoa dhabihu za kifedha kwa kawaida alipunguzwa kutoka kazini kwake. Muda kidogo baadaye, aliugua na ikabidi anunue dawa za bei ghali. Alikuwa na wasiwasi sana kutokana na hali yake ya kifedha. Siku moja, akijua kwamba hakuna kitu ndani yake, aliamua kuangalia salio kwenye kadi yake ya benki, na kwa mshangao wake, alikuta kuna pesa kiasi cha 190,000 fedha za huko katika akaunti yake ya benki. Aligundua kuwa kampuni yake ya zamani ilikuwa imemuwekea pesa hizo kwenye akaunti yake kama zawadi kwa bidii na uaminifu ambao alionyesha wakati wa kazi yake.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba mtu mmoja kutoka Senegal hakuwa na fedha za kutimiza ahadi yake ya Tahrik-e-Jadid kwani mwaka ulikuwa unaelekea mwisho. Hata hivyo, alisema kuwa bila shaka atatoa kiasi alichoahidi, hata kama ingemaanisha kuuza nguo zake. Siku chache baadaye, alienda kwa mbashiri wa eneo hilo na kumwomba apokee dhabihu yake ya kifedha. Alisema kwamba kwa namna fulani, bila kutarajia, binti yake alimtumia pesa, ambazo zilimwezesha kutimiza ahadi

Ukurasa 4

Imani na Dhabihu ya Kifedha: Uzinduzi wa Mwaka wa Tahrik Jadid

Kutoka Uk 3..

yake ya Tahrik-e-Jadid.

Huzur Aqdas (atba) alisema kwamba Ahmadiyya mpya nchini Tanzania alikuwa ametoa ahadi kubwa kwa ajili ya Tahrik-e-Jadid. Alikuwa mkulima, na kutokana na kutokuwa na mvua, hakukuwa na mazao mengi. Alikuwa na wasiwasi sana jinsi atakavyoweza kutimiza ahadi yake. Siku moja, alipokea simu kutoka kwa rafiki yake wa zamani ambaye hakuwa amezungumza naye kwa muda mrefu sana, ambaye alisema kwamba anamtumia pesa kiasi fulani. Baada ya kupokea kiasi hicho, alikwenda moja kwa moja kwa mbashiri wa eneo hilo na kutimiza ahadi yake kwa ajili ya Tahrik-e-Jadid.

(Hii ni mifano michache tu ya matukio mbalimbali yaliyotajwa na Huzur Aqdas (atba))

Madhumuni ya Kuanzishwa Tahrik-e-Jadid

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba hii ndiyo namna ambayo hata Waahmadiyya wapya wameanzisha ari ya kujitolea fedha. Je, majaribio ya wapinzani wa Ahmadiyya yanaweza kuzima nuru hii ambayo imewashwa na Mungu? Wanaweza kujaribu kadiri wawezavyo, lakini mwisho wa wapinzani wa Ahmadiyyat umekusudiwa kuwa kushindwa na kufadhaika.

Huzur Aqdas (atba) alisema kwamba Tahrik-e-Jadid ilianzishwa katika wakati ambapo Jumuiya ya Ahmadiyya ilikuwa inakabiliwa na upinzani kutoka pande zote. Taasisi hii iliundwa kwa lengo la msingi la kueneza ujumbe na hivyo kupanua Jumuiya ya Ahmadiyya ili kuinua bendera ya Uislamu katika kila nchi ya dunia. Ni katika roho ya kushikilia kusudi hili kwamba tunapata mifano kama hii ya dhabihu za kifedha leo.

Huzur Aqdas (atba) alisema kwamba harakati ya Ahrar imedai kwamba wataiondoa Ahmadiyya kutoka kwenye uso wa dunia; wangeondoa Qadian na walikuwa wamefanya mipango ya kuchafua maeneo mbalimbali, likiwemo kaburi la Masihi Aliyeahidiwa (as). Badala ya kuzuiwa na serikali, wangeungwa mkono nao. Ilikuwa chini ya mazingira haya ambapo Khalifa wa Pili alibuni mpango kwa ajili ya Jumuiya, ambao sehemu yake ilikuwa ni kutoa mhanga wa kifedha. Matokeo yake, wanachama wengi waaminifu wa Jumuiya walianza kumwandikia Khalifa wa Pili mara moja kwamba walikuwa tayari kutoa dhabihu yoyote inayohitajika. Kisha, Khalifa wa Pili akatangaza rasmi kuundwa kwa mfuko kwa ajili ya kujibu mashambulizi dhidi ya Jumuiya kwa kueneza ujumbe wa Uislamu Ahmadiyyat. Wakati huo, lengo lilikuwa kukusanya Rupia 27,000 katika miaka mitatu. Walakini, shauku ya wanachama wa Jumuiya ilikuwa hivi kwamba kiasi cha Rupia 100,000 kilikusanywa ndani ya kipindi cha mwaka mmoja tu. Roho hiyo ya dhabihu haikubakia kwao tu, kwani sasa roho hiyohiyo ya dhabihu inashuhudiwa ulimwenguni pote.

Awamu za Mpango wa Tahrik-e-Jadid

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba mwanzoni, Khalifa wa Pili (ra) alirefusha mpango huu kutoka miaka mitatu hadi miaka kumi. Hata hivyo, baada ya kuona shauku na bidii inayoongezeka ambayo wana Jumuiya waliendelea nayo kujitolea, mpango huu ukawa msingi wa kudumu.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba kulikuwa na watu 5,000 ambao mwanzoni walijitolea mhanga chini ya mpango huu na hivyo kuwa sehemu ya Daftar Awwal (awamu ya 1). Baada ya miaka kumi, Khalifa wa Pili (ra) alianzisha Daftar Daum (awamu ya 2), muda ambao aliweka kuwa miaka 19, na kisha akatangaza kwamba Daftar mpya itaanzishwa kila baada ya miaka 19. Kisha, Daftar Siwam (awamu ya 3) ilitangazwa na Khalifa wa Tatu (rh), lakini kuanzishwa kwake kulihusishwa na Khalifa wa Pili (rh) pia. Kisha Daftar Chaharam (awamu ya 4) ilianzishwa na Khalifa wa Nne (rh). Kisha, mwaka wa 2004, Daftar Panjam (awamu ya 5) ilianzishwa na Khalifa mtukufu wa Tano (atba). Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alitangaza kwamba leo, baada ya kukamilika kwa miaka mingine 19, anatangaza kuanzishwa kwa Daftar Shasham (awamu ya 6) na wanachama wote wapya na watoto lazima sasa waainishwe chini ya kitengo hiki.

Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema kwamba namna ambavyo wale wanaotoa dhabihu za kifedha kwa ajili ya Tahrik-e-Jadid wanabarikiwa inathibitisha kwamba huu ni mpango wa kiungu. Hadhrat Khalifatul Masih (atba) alisema pia kuna nafasi ya kuboreshwa ambapo wale waliobarikiwa na mali wanaweza kuongezeka katika dhabihu zao.

Huzur Aqdas[atba] alisema kwamba leo hii, idadi ya misikiti yetu katika nchi 220 za dunia ni zaidi ya 9,300. Idadi ya nyumba za misheni ni zaidi ya 3,400. Kuna makumi ya misikiti na nyumba za misheni zinazojengwa kwa sasa. Idadi ya wamisionari na mu'allimeen (walimu) duniani inakaribia 5,000 na inaongezeka. Qur'an Tukufu imetafsiriwa katika lugha 77. Maandiko katika lugha mbalimbali yanaendelea kuchapishwa na kazi nyingine nyingi pia zinafanywa kupitia Tahrik-e-Jadid pamoja na mifumo mingine.

Tangazo la Mwaka wa 90 wa Tahrik-e-Jadid

Huzur Aqdas (atba) alitangaza kwamba mwaka wa 89 wa Tahrik-e-Jadid ulifika tamati yake na kutangaza kuanza kwa mwaka wa 90. Katika mwaka uliopita, Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya duniani kote ilitoa dhabihu ya pauni milioni 17.20, ongezeko la zaidi ya £700,000 ikilinganishwa na mwaka jana. Hii ni licha ya hali ngumu ya kifedha duniani. Kando na Pakistan, nafasi za nchi kulingana na michango yao ni kama ifuatavyo:

1. Ujerumani, 2. Uingereza, 3. Canada, 4. Marekani, 5. Nchi ya Mashariki ya Kati, 6. India, 7. Australia, 8. Indonesia, 9. Nchi ya Mashariki ya Kati, 10. Ghana.

Kwa nchi za Afrika inayoongoza ni Ghana, kisha Mauritius, Nigeria, Bukinafaso, Tanzania, Gambia, Uganda, Liberia, Seraleon na Benin.

Nchi ambazo zimeongeza idadi ya wachangiaji ni Geaneaconerkry, Jamaica, Kirigstan, Zambia, Nepal, Ghana, Kenya, Tanzania, Congo Kinshasa, Congo Brazaville, Nigeria, Senegal, Ivory Coast na Jamaat moja ya Mashariki ya Kati.

Khalifa mtukufu (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu awabariki wale wote ambao wametoa dhabihu za kifedha na kuwawezesha kuendelea kutoa dhabihu kubwa zaidi katika siku zijazo.

Khalifa mtukufu[atba] alihimiza: Tusiwasahau Wapalestina katika sala zetu. Huzur Aqdas (atba) aliomba kwamba Mwenyezi Mungu Ajaalie haraka njia za kuwakomboa kutokana na dhulma kubwa ambayo wanawake na watoto huko Palestina wanakabiliana nayo.

Yesu aliongozwa na nani Nyikani?

Kutoka toleo lililopita

HIKI NI KIKOSI KAZI CHA WANAFIKI W A L I O W A P O T E Z A WATU NA KUIACHA IMANI SAHIHI ILIYOFUNDISHWA NA YESU.

(1) Yuda Iskariote
(2) Petro wa (kefa);
kefa maana yake ni jiwe (mgumu kuelewa).
(3) Yakobo
(4) Paulo, (sauli)
(5) Barnaba
(6) Anania, nk.

Yuda alimsaliti mwalimu wake kwa vipande thelathini tu, vya fedha.

Petro ni mnafiki tu, (Gala 2:11)

Petro alimkana mwalimu wake mara tatu.

Petro aliwafundisha Wayahudi sheria ya MUNGU Lakini mwenyewe hakutaka kuifuata.

Paulo haieleweki majukumu alipewa na nani kule Damaskasi Kati ya Anania au YESU.

Paulo alijiamulia tu mwenyewe kwenda kwa watu wa mataifa mengine. mdo 18:5--6;

Paulo aliwazuia watu kuifuata sheria ya Musa na desturi yake ya kutahiriwa. mdo 21:21 na 27;21--28; na kuiita sheria ya MUNGU ni laana, na huwezi kuhesabiwa haki kwa kuifuata sheria.

Paulo alionyesha unafiki mkubwa katika swala la IMANI yake, akienda kwa washirikina nae anakuwa sawa nao, kwa watu wa mataifa vivyo hivyo, wasiojua sheria nae pia, nk, 1wakor 9:19--21; pia ni mbabaishaji tu, mara Myahudi mara Mtaliano, sura ya 21:28;

Ili awapate wafuasi wake, Yesu hakufanya hivyo.

Hata Yakobo aliyekawa na msimamo na IMANI safi kabisa na kuweza kufafanua maana ya IMANI, ukisoma kitabu chake, sura zote tano ni safi tu. Lakini akazolewa na wahuni na UNAFIKI wa Paulo na Petro akatoa maamuzi mabaya sana ya kupunguza sheria kumi na kuwapa watu wa mataifa mengine sheria nne tu,

Na kikao hicho kilifanyika kule Yeluselemu tena walikusanywa na wazee wa mji ule. katika barua hiyo aliyoiandika na kufanya maamuzi hayo inapatika katika kitabu cha matendo, mdo 15:1--33;

Kwa sababu hiyo mimi naamua hivi; Tusiwataabishe wale waliomgeukia Mungu katika Mataifa;

bali tuwaandikie kwamba wajiepushe na unajisi wa sanamu, na uasherati, na nyama zilizosongolewa, na damu.

Kwa maana tangu zamani za kale Musa anao watu wahubirio mambo yake; katika kila mji husomwa kila sabato katika masinagogi.

Basi ikawapendeza mitume na wazee na kanisa lote kuwachagua watu miongoni mwao na kuwapeleka Antiokia pamoja na Paulo na Barnaba; nao ni hawa, Yuda aliyeitwa Barsaba, na Sila, waliokuwa watu wakuu katika ndugu. Wakaandika hivi na kupeleka kwa mikono yao,

Mitume na ndugu wazee, kwa ndugu zetu walioko Antiokia na Shamu na Kilikia, walio wa Mataifa; Salamu.

Kwa kuwa tumesikia ya kwamba watu waliotoka kwetu wamewasumbua kwa maneno yao, wakipotosha roho zenu, ambao sisi hatukuwaagiza;

sisi tumeona vema, hali tumepatana kwa moyo mmoja, kuwachagua watu na kuwapeleka kwenu pamoja na wapendwa wetu Barnaba na Paulo,

watu waliohatirisha maisha yao kwa ajili ya jina la Bwana wetu Yesu Kristo.

Basi tumewatuma Yuda na Sila, watakaowaambia wenyewe maneno yayo hayo kwa vinywa vyao.

Kwa maana ilimpendeza Roho Mtakatifu na sisi, tusiwatwike mzigo ila hayo yaliyo lazima,

yaani, mjiepushe na vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, na damu, na nyama zilizosongolewa, na uasherati. Mkijizuia na hayo, mtafanya vema. Wasalamu. mdo 15:19--29

Wamepunguza sheria (Amri) kumi za MUNGU.

Na nyayo hizo zinaendelezwa na kanisa KUU la Romani katholiki na makanisa mengineyo,

kufuta maandiko wasiyoyapenda kwa sababu ya imani yao, na kuongeza yanayoendana na imani yao. na unaposoma Biblia utaona vifungo vya mraba hivyo vimechomekwa tu.

na mfalme consantino pia aliongeza UPAGANI huo.

KWA MAANA HIYO WAKRISTO WA LEO W A M E Y A A C H A M A F U N D I S H O SAHIHI YA YESU, NA KUYAKUMBATIA YA UPAGANI.

NDIO MAANA YA YESU KUONGOZWA NA SHETANI NYIKANI, (POLINI).

EWE MKRISTO TUMIA MAARIFA (AKILI), ULIYOPEWA NA BWANA MUNGU WAKO KUJIONDOA KWENYE MAKUCHA YA SHETANI ILI UINGIE KWENYE UFALME ULIOAHIDIWA.

TORATI HAIKUJA ILI KUIONGOZA DUNIA LA; NI KWA WANA WA ISRAEL TU. KUNA MKUU WA ULIMWENGU HUU AMEKWISHA HUKUMIWA, NDIE WA KUMPOKEA HILO NDILO AGIZO LA YESU. YUDA 1:14--15 NA YOHANA 16:8--14;. MWENYE MASIKIO NA ASIKIE.

Aliyekuja na mwongozo (kitabu) kwa WATU WOTE tangazo lake ni hilo hapo chini,

Sema; Enyi WATU, Kwa hakika mimi ni Mtume wa mwenyezi mungu kwenu nyoote, ambaye Anao ufalme wa mbingu na Ardhi, hapana aabudiwaye ila Yeye, Ahuishaye na Afishaye, basi muaminini mwenyezi mungu na mtume wake aliye Nabii ummi ambaye humwamini mwenyezi mungu na maneno yake; na mfuateni yeye ili mpate kuongoka.(Kuran 159;7)

Ambao wanamfuata mtume, Nabii aliye Ummi, ambaye wao humkuta ameandikwa kwao katika Taurati na Injili, Huwaamuru yaliyo mema na huwakataza yaliyo mabaya, na huwahalalishia vitu vizuri na huwaharamishia vitu vibaya, na huwaondolea mizigo yao na minyororo iliyokuwa juu yao,

Ama wale waliomuamini yeye na kumheshimu na kumsaidia na wakaifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye, hao ndio wenye kufauru. (7:158)

Mwanga umeangaziwa milima ya Farani (Taurati 3-33:2)

Enyi WATU wa kitabu! bila shaka amewafikieni mtume wetu, huwabainishieni katika wakati usio na mitume, msije mkasema, hakufika kwetu mtoaji wa habari njema wala mwonyaji; Kwa hiyo amewafikieni Abashiriaye na aonyaye, na Mwenyezi Mungu Anao uwezo juu ya kila kitu. 5:20;

Baada ya kuachwa na ukiwa takribani MIAKA mia sita, (600); wakati haikuwa hivyo unapoisoma desturi ya MUNGU.

NA NENO LANGU LA MWISHO NI UPENDO KWA WOTE BILA YA CHUKI KWA YEYOTE.

Bustani ya Washairi

Masharti ya Baiati.
Kwa jina lake Manani, jina la Mola muweza
Alonipa umakini, bayana ninaeleza
Kwa beti hizi amini, mwongozo unafatiza
Mashariti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

Nianze nalo la kwanza, alotuasa Masihi
Allah kumuweka kwanza, hakuna anoshabihi
Shiriki itatuponza, kwa sababu haiswihi
Masharti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

Pili kusema ukweli, kuzitimiza ahadi
Tuukwepe ufidhuli, uasi na ufisadi
Tuziepuke ghuruli, katuambia Mahadi
Masharti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

Sala tano tuzisali, hata nayo Tahajjudi
Kumsalia Rasuli, jamani tujitahidi
Ghofira kwake jalali, kuomba hatuna budi
Masharti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

Tusiwadhuru viumbe, alowaumba mwenyezi
Tusijione vijembe, kufanya ya kipuuzi
Nafsi tusizipambe, kwa tamaa za kishenzi
Masharti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

Tuzikubali kudura, zitokazo kwa mwenyezi
Na tujitoe kafara, kwenye njia ya Azizi
Sote tuwe wa Shakira, kwa amri zake mwenyezi
Masharti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

Tuziache desturi, zile zisizo maana
Na tuzifate amri, alotuasa Rabanna
Mtume zake amri, tuzifate tutafana
Masharti ya bayati mwongozo ulotukuka

Tukiepuke kiburi, hata nayo majivuno
Tutende yalo mazuri, nayo mazuri maneno
Huruma ni jambo zuri, ili tuwe wa mfano
Masharti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

Na kuifahamu dini, pia na kuiheshimu
Tuione ni ya shani, dini ya Uislamu
Dini ni bora jamani, na hilo tulifahamu
Masharti ya bayati, mwongo ulotukuka.

Kuhurumia viumbe, kwa ajili ya Manani
Nyoyo zetu zisivimbe, kufanya ufirauni
Tuwapendeni viumbe, Masihi katuauni
Masharti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

La mwisho hili sharti, la kumi namalizia
Tuwe na moyo thabiti, ahadi kutimizia
Kuyatii masharti, pia tuifate njia
Masharti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

Kaditama sio mbizi, ninarudi darasani
Mi sijaota mizizi, katika ushairini
Siwezi piga mruzi, bado mimi ni kindani
Masharti ya bayati, mwongozo ulotukuka.

Sharif A. Nyamihasi
Ahmadiyya Jamaat Kagenyi-Kagera.

Habari za Kuondoka

Wamba sikuzifikisha, habari za kuondoka
Usiku kucha wakesha, lawama ukinitwika
Ukweli unapindisha, taarifa ilifika
Ilikuwa ni ya fumbo, na mwelevu hufumbua.

Yatafakari maisha, fumbo lilivyofichika
Nywele zilikujulisha, kwa kule kubadilika
Ukahusudu tamasha, pasi kujali mipaka
Hizo bati za kichwani, ni za nyumba ya milele

Meno yalichangamsha, hususa ulipocheka
Hivi leo unatisha, ni mengi yameshangoka
Sasa mithili ya kasha, bidhaa zinadondoka
Kasha linahadhi gani, bidhaa zikidondoka?

Tama mifano yatosha, alolala kuamka
Jaribu kuunganisha, Taa yako itawaka
Siraja ikishawasha, na giza linatoweka
Kipi cha kuzidi Nuru, kwa utukufu na shani?

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)
Kiwalani - Migombani.

AKIBA YATEKETEA

Akiba niloiweka, kikapuni nikatia
Miaka yakupigika, nipate chakuendea
Siku itakapofika, nisibaki najutia
Shetani waitumia, dhambini unanitia

Shetani waitumia, dhambini unanitia
Hasara nibakishia, thawabu zikapotea
Nini nitakichukua, siku takapo wadia?
Deni lisilolipika, shetani unanitwika.

Deni lisilolipika, shetani unanitwika
Ahadi sokamilika, hauachi kuziweka
Eti nitanufaika, dunia nikiishika
Kifo wanisaulisha, Ili nije kujutia

Kifo wanisaulisha, Ili nije kujutia
Muda utakapoisha, Sina chakukichukua
Dunia lonipotosha, niiache nikilia
Nakuomba mola wangu, nijalie mwisho mwema

mtunzi
Masihi Omary stambuli kisagwa

MOLA WETU TULINDE

Shetani hajatwacha, tupate kutulia
Wovu huu kiacha, mwingine sogezea
Hataki kutuacha, nafsi zikatulia
Mola wetu tulinde, sirudi likotoka.

Mtunzi
Masihi Omary Stambuli Kisagwa

Heri Shari ni vyake

Salamu alekumu, pole sana ndugyangu
Mekukuta magumu, maumivu uchungu
Vumilivu muhimu, kwenye haya machungu
Usimkufuru mungu, heri Shari nivyake

Mtunzi
Masihi Omary stambuli kisagwa

UPENDO KWA UKHALIFA.

Ewe mwenye Nuru tele,Mkidhi wa kila haja
Ulo hai wa milele,Mujibu wa kila hoja
Muinua wateule,Mpandisha madaraja
Tupandie mioyoni,Upendo kwa Ukhalifa

Ukhalifa ni neema,Bada ya unabii
Ausimika karima,Kwa wale wanaotii
Kwao dini husimama,Pinzani hawahofii
Matumaini twapata, Upendo kwa Ukhalifa

Tuupende Ukhalifa, Kwa roho bila kikomo
Kwani hapendi hafifa, kwenye kilo wala kimo
Huba rahaye kufa, Hilo nakupa ni somo
Daima tuupe haki, Upendo kwa Ukhalifa

I sauti ya uhai,Ndaniye roho hushiba
Hulevya kama divai,Hudumisha unasaba
Tukuze yetu jamii, tunae mmoja baba
Tushike imara kamba,Upendo kwa Ukhalifa

Dua zetu kwa Khalifa,tuzitilie mkazo
Maombi nusu kufa, hupita bila mzozo
Tumtakie kaifa, salamu haina tozo
Tuitambue thamani, Upendo kwa Ukhalifa

Tuwe tayari jitoa,Kwa nukudi na kadiri
Dini tuweze okoa,Toka mikono hatari
Watu tuweze ongoa,Kwa mapenzi na Johari
I mbele taa yetu,Upendo kwa Ukhalifa

Tufanye usaidizi, wenye jazba na hofu
Nasi tuzipande ngazi,Kwa huba na uongofu
Tuviongozi vizazi,Viepukane na ufu
Daima uwe imara, Upendo kwa Ukhalifa.

Shunda Mshundia Wana
Morogoro.

ALIYA

Tumepokea Salamu, manyoni zina tokea
Kuwa Aziza mudhamu, Mwana amejifungua
Tena Mwana lomuhimu, wakfu wa Jumuia
Karibu wetu mgeni, mtoto wetu ALIYA

Ni baraka za kudusi , Mola ilahi Rabuka
Tuna kushukuru sisi, na Saidi Mgeleka
Ilikua si rahisi, machozi kutiririka Karibu
wetu mgeni, mtoto wetu ALIYA

Yahitajika nidhamu, Mwana huyu kumleya
Sote tunalo jukumu, wazazi ndugu pamoya
Tumpatie elimu, Mola Anayoridhiya
Karibu wetu mgeni, mtoto wetu ALIYA

Muumba wangu Rabuka, Mwana huyu msitiri
Kwako mimi sina shaka, mzidishie ya kheri
Utampa nayo taka, kila aombapo zuri
Karibu wetu mgeni, mtoto wetu ALIYA

Rajabu Abasi Mkieti (Al-Wattani _Mlezi)
Lusanga Muheza Tanga

Jeshi limeongezeka, Karibu katika nyumba
Aliya twafurahika, dua twazidi kuomba
Uwe mwana wa baraka, ukue Kama mgomba
Hatimaye ujiunge, kwenye jeshi la Masihi

Mhariri

RADHI

Kweli safari ya tabu, kuipata yake radhi
Kumfikia Wahabu, funga Sunna na faradhi
Ili kuchuma zabibu, ushike huno waadhi
Safai hino ni ndefu, yahitaji masurufu

Mahmood Hamsin Mubiru (Wa Mamba)

Upendo

Mwanaume mmoja alimuoa mwanamke mrembo. Alikuwa akimpenda sana. Siku moja mwanamke alipatwa na maradhi ya ngozi. Kidogokidogo alianza kupoteza urembo wake.

Mume alipata safari na wakati akirudi alipata ajali iliyomfanya apoteze uwezo wake wa kuona. Hata hivyo, maisha yao ya ndoa yaliendelea kama kawaida. Lakini kadiri siku zilivyosonga mbele ndivyo mke alivyoendelea kupoteza urembo wake. Kwa kuwa mume alikuwa kipofu hakulijua hilo na hivyo hakuna kilichobadilika kwenye upendo wao. Aliendelea kumpenda, na mke alimpenda sana mumewe.

Siku moja mke alifariki dunia. Ilikuwa huzuni kubwa sana kwa mume.

Baada ya kumaliza taratibu zote za maziko, mazishi na kutandua msiba, alipanga kuhama kwenye mji huo na kwenda kuishi kwenye mji mwingine.

Mtu mmoja aliposikia habari hiyo alimwendea na kumuuliza: ?Sasa utawezaje kutembea peke yako? Maana siku zote hizi mkeo alikuwa akikusaidia kukuonesha njia.?

Akajibu: Mimi si kipofu. Nilifanya ionekane hivyo kwa sababu angejua kwamba ninauona mwili wake ulivyobadilika kuwa mbaya angepata maumivu makubwa zaidi kuliko ugonjwa wake wenyewe. Alikuwa mke mwema sana. Nilitaka aendelee kuwa na furaha.

FUNZO:

Wakati fulani ni vizuri ukajifanya kipofu na kuyapuuza mapungufu ya mwenzako ili kumfanya awe mwenye furaha .

Meno huung?ata ulimi mara nyingi, lakini vinaendelea kuishi pamoja kinywani. Huo ndio moyo wa KUSAMEHEANA. Macho hayaonani, lakini yanatazama na kuona vitu kwa pamoja, hupepesa na kulia pamoja. Huo unaitwa UMOJA.

Ukiwa peke yako unaweza kuongea, lakini ukiwa pamoja na mwenzako mnaweza KUZUNGUMZA.

Ukiwa peke yako unaweza KUFURAHI, lakini ukiwa na mwenzako unaweza KUFURAHIA

Ukiwa peke yako unaweza KUTABASAMU, lakini ukiwa na mwenzako mnaweza KUCHEKA.

tazama nakumbuka kuwa Kiwembe kina ukali lakini hakiwezi kukata mti; shoka lina nguvu na imara lakini haliwezi kukata nywele hivyo vyote kiwembe na shoka vina umuhimu wake kwa mahala pake

Kila mtu ni muhimu kulingana na kusudio na lengo la uwepo wake. Usimdharau mtu yeyote kwa hali yoyote, kwa sababu huwezi kuwa yeye kwa vyovyote na pia amini kuwa upo umuhimu wa uwepo wake .

Mwenyezi Mungu atujaalie nguvu na moyo wa kusamehe, kustahimiliana na kuishi kwa umoja na upendo .

Kurani Tukufu kwenye Kilele cha Mlima Kilimanjaro

...Kutoka uk.11

na urefu wa mita 100. Watalii wageni wakija kupanda mlima Kilimanjaro lazima watajitahidi wafikie kilele cha taifa Uhuru Peak. Mtalii anaweza kukosa nguvu ya kuendelea, viongozi watafanya kazi ya ziada kumpulizia ili apate nguvu ya kufika Uhuru Peak. Sisi waislam wa Ahmadiyya kazi yetu iliishia hapo Gilmans Point. Tumekuwa washindi wa kupanda mlima wowote duniani, kuthibitisha ushindi huo tulipata cheti maalum, ambacho kimehifadhiwa huko Uingereza makao makuu ya Jumuiya ya Ahmadiyya Duniani. Bila kusahau wale marafiki zetu wajerumani, walitupiga picha ya pamoja tukiwa kituo cha Horombo Halt, picha walitupelekea walipofika Ujerumani.

Kuteremka Mlimani.

Tulipoweka sahihi na Kurani yetu ya mwisho, hatukuruhisiwa hata dk5 kuangalia au kupiga picha. Mara moja tuanza kurudi. Hadi pale Kibo Halt. Ushukaji sio kutembea bali kujirusha na kufikia kisigino. Njia hii tulitumia saa 1 kutoka Gilmans Point hadi Kibo Halt. Tulifika Kibo Halt salama tulifurahi sana na tulinunua soda kwa furaha hiyo.

Safari toka Kibo Halt hadi Horombo Halt.

Baada ya kufaulu kufika kilele cha kwanza, tukajipongeza kwa kunywa Soda kana kwamba inatoka ndani ya Friji. Tulikunywa hivyo hivyo ndipo tukaambiwa yule mwenzetu amerudishwa kwa machela hadi Horombo Halt bila shaka mtamkuta huko. Tulijiandaa na wapagazi wetu hadi Horombo Halt. Tulimkuta Marhun Mzee Mwishehe Juma akiwa na afya njema na aliongeza maneno mwenyewe ifuatavyo. Ndugu zangu nashukuru mmenikuta sijambo, ila hiyo homa iliyonikuta, katika maisha yangu haijawahi kunikuta kama hiyo. Maana nilishindwa kuvaa hata nguo bali nilivalishwa, lakini sasa kituo hiki hali ya hewa yake ni nzuri sijambo. Tukalala hapo Horombo Halt ni siku ya nne hadi kesho siku ya 5 tukaitisha safari yetu.

Horombo Halt hadi Marangu National Park - Ofisini.

Ilikuwa tarehe 27/03/1989 saa 3 asubuhi, tulianza safari ya kupanda mlima Kilimanjaro. Tuliwasuli ofisi za kitalii saa 5 kamili, tukarudisha vifaa vyote tulivyokodi. Mafisa utalii walimhoji kiongozi wetu kuwa nani amefika Gilmans Point, naye akathibitisha kuwa ni sisi wawili. Bahati mbaya mmoja wetu Mzee Mwishehe Juma alipata homa kali. Mafisa wakasema amejitahidi kufika Kibo Halt, maana wengine hawafiki pale wanaishia mwanzoni tu.

Wakati tupo njiani kutoka Mandara hadi Marangu National Park. Tulikutana na wanafunzi wa shule ya Sekondari Tambaza wakielekea kituo cha Horombo Halt. Wengi wao walionekana wamechoka mapema. Hivyo tulikabidhiwa ushindi wa pili wa kupanda mlima Kilimanjaro. Tulimkuta mwenyeji wetu ili atupeleke na kutufikisha kituo cha reli kurudi Dar es Salaam. Tulipokuwa safarini tukapata habari kuwa mvua iliyonyesha leo huko Mlimani, haijapata kunyesha kiasi hicho zaidi ya miaka 35 iliyopita, na tayari mwanafunzi mmoja amefariki dunia. Tukamshukuru sana Allah wa kusikia maombi yetu. Mvua ilifunga siku tano mfululizo. Nilitunga utenzi kumshukuru Allah. Nilianza kuimba kama ifuatavyo.

Mara tumefika Moshi
Tukasikia Tamshi
Mvua imeua Mushi
Kurani Kileleni

Uchagani kukavuma
Ahamadiya Kalima
Muhamadi Mu-Adhama
Kurani Kileleni

Siku tano kuanguka
Mvua isiyokatika
Kazi yetu kamilika
Kurani Kileleni

Tukaingia Ngorongoro
Tereni yetu kwa ringo
Usafiri hadi Bongo
Kurani Kileleni

Twamshukuru Rabuka
Kutuwezesha kufika
Kileleni muafaka
Kurani Kileleni.

Kuiendea Elimu na matumizi yake yenye Baraka kwa mujibu wa Islam

Na. Swaleh Kitabu Pazi

...Kutoka toleo lililopita

shaka hujitokeza pindi tadbiir inapofanyika. Hadhrat Ahmad[as] kadhalika ameelezea jambo hili alipoandika kuwa;

Hapa pia panaashiria kwamba mtu anapotenda tendo fulani, Mungu naye. Anatenda tendo moja kuwa matokeo ya tendo la mtu yule. Mathalan, mtu anapofunga milango yote ya chumba chake, Mwenyezi Mungu Analeta tendo lake la kutia giza chumbani humo. kwani mambo yote yaliyo matokeo ya matendo yetu kwa kulingana na sheria ya ulimwengu iliyowekwa na Mungu,

ndiyo matendo ya Mungu. Maana Yeye ndiye Huleta matokeo yote. (***Hekima ya Mafundisho ya Kiislam, uk. 112***).

Kwa hali hii tunapaswa kufahamu kuwa, kwa mujibu wa Islam, kuiendea elimu kunahitaji sana matendo na juhudi zetu ili tuweze kushawishi matendo ya Allah katika kutupatia mwongozo. Basi ni vyema tutie bidii kubwa katika utafutaji wa elimu huku tukiendelea kuomba dua hii; rabbi zidnii 'ilma war zuknii fahma – Mola wangu uniongezee elimu na uniruku ufahamu.

Kwa mujibu wa maelezo ya Masihi Aliyeahidiwa[as] ni kwamba Allah ndiye chanzo cha elimu zote. Ukweli huu bila shaka unabainishwa pia kupitia Qur'an Tukufu, ambayo inatueleza kwamba Allah ndiye aliyemfundisha mwanadamu elimu zote alizo nazo. Humo Allah anatajwa kuwa;

Al ladhii 'allama bil qalam, 'allamal insaana maa lam ya'lam

Ambaye Alifundisha kwa njia ya kalamu. Alimfunza mwanadamu mambo asiyoyajua. (96:5-6).

Hivyo kwa mujibu wa nadharia ya kiislam ni kwamba, elimu yoyote ya kweli ni lazima iwe imetoka kwa Allah, hata kama itapatikana duniani kupitia kwa watu wanaoonekana kuwa si wenye ukaribu na Allah. Waislam wameshauriwa kuitwaa elimu popote watakapo wajihiana nayo, maana kimsingi hiyo ni haki yao iliyowaponyoka kutokana na sababu moja au nyingine. Mtume Mtukufu saw anasema kuwa;

Al kalimatul hikmatu dwallatul mu-min, fa haithu wajadahaa fahuwa ahaqqu bihaa. Neno la hekima ni mali ya muumini ilyopotea, hivyo popote aikutapo hiyo ni haki yake. (Tirmidhi, Kitabul 'Ilm).

Neno la hekima hapa humaanisha elimu, na kwa mujibu wa mafundisho ya Islam, elimu hasa ni ile yenye manufaa kwa watu, ni tasnia inayoweza kunawirisha ufahamu wa watu badala ya kuufubaza, na kukuza akili za watu badala ya kuzidumaza. Ndiyo maana hata waislam wa mwanzo, baada ya kunawirishwa kiroho kwa ujio wa Mtukufu Mtume saw, walipiga hatua kubwa za kielimu.
Kupitia mafundisho ya Qur'ani Tukufu na hadithi za Mtume saw, waislam walijifunza mengi juu ya dini, Sanaa na utamaduni. Lakini pia walipata elimu nyingi za kimantiki na kifalsafa na kisayansi, ambazo ziliwafanya wathibitike kuwa umati bora uliotolewa kwa ajili ya watu. Hata hivyo hawakupuuza elimu yoyote iliyowajia, hata kama ilitokana na watu wasiokuwa waislam.

Ni kutokana na dhana hii ndiyo maana tunakuta kwamba, hata elimu za kale zilizofundishwa na wana falsafa na wana sayansi wa kigiriki zilifasiriwa, zikaboreshwa na kusambazwa na wasomi wa kiislam. Watu kama Ibn Rushd, Ibn Sina, Razi, Ghazal na wengineo, waliibuka kuwa wafasiri na waboreshaji wakubwa wa nadharia mbalimnbali za kielimu zilizofundishwa na akina Socrates, Aristotle, Galen na Plato. Kupitia harakati za utafiti na usambazaji wa elimu zilizofanywa na waislam wa mwanzo, sawa na maagizo ya Mtume Mtukufu[saw], Nuru ya elimu ikatandawaa duniani. Asia, Afrika na Ulaya.

Zikanawirishwa na ustaarabu mpya wa kielimu ulioletwa na waislam. Ni kupitia ukufunzi wa waislam ndipo hata nchi za ulaya zilipata kuamka kielimu na hatimaye kujiendeleza hadi katika hali ziliyo nayo sasa.

Hata wasomi wa kimagharibi wanakiri kwamba, kwa ujio wa Muhammad[saw], waislam waligeuka kuwa wasambazaji wakuu wa elimu ya kale iliyokuwa imesahaulika. Hili linathibitishwa na Prof. William Montgomery Watt, Mtaalamu wa historia na mambo ya kimashariki kutoka uskochi, aliyekuwa profesa wa masomo ya kiarabu na kiislam katika chuo kikuu cha Edingburg, Scotland.
Aliyeandika katika kitabu chake Influence of Islam in Medieval Europe kwamba;

"one sees that without the arabs european science and phylosophy would not have developed when they did..... and the europeans had to learn all they could from the arabs before they themselves could make further advances".

Mtu huona kwamba bila ya waarabu sayansi na falsafa ya Ulaya haingeweza kuendelea kama ilivyofanya..... na wazungu walipaswa kujifunza yote waliyoweza kutoka kwa waarabu, kabla wao wenyewe kujiendeleza baadaye. (uk 43)

Ni dhahiri kwamba Islam haikuwahimiza waumini wake kutafuta na kusambaza

elimu juu ya theolojia pekee. Hivyo waislam hawakujikita katika usomi wa fiq-hi, taswauf na aqaaid pekee, bali pia elimu za sanaa na sayansi zilisomwa na kusambazwa kama sehemu za mafundisho ya dini. Ndiyo maana tunakuta kwamba matabibu, wakemia, wana hisabati, wana fizikia na wana falsafa wengi wa mwamzo wa kiislam, walikuwa ni wanazuoni wakubwa wa kidini. Baadhi yao walikuwa ni mawalii wa kutajwa katika Islam. Ni jambo la kushangaza kuona leo hii, kuna makundi yanayojiita kuwa ni ya kiislam, yanayoeneza nadharia zinazowaweka waumini wao mbali na elimu ya kisekula. Bila shaka jambo hili ni geni katika Islam na wala halina msingi wake katika mafundisho ya Mtume Mtukufu, Muhammad[saw].

Profesa Abdus Salaam, mwana sayansi wa kwanza wa kiislam kushinda tuzo ya Nobel, aliwahi kueleza katika moja ya mihadhara yake kwamba; katika Qur'ani Tukufu yenye aya zaidi ya 6000, ni aya 250 tu ndizo zinazoamrisha juu ya mambo ya ibada kama vile kusali, kufunga, kutoa zaka, kuhiji na kutekeleza baadhi ya amri za kidini. Lakini aya nyinginezo, zimejikita juu ya masuala mengi mtambuka ya kimaisha. Ikiwa ni pamoja na kuchunguza na kutafakari juu ya maumbile, kutafiti juu ya historia na kutalii tabia na maisha watu nk. Bila shaka hizi ni tasnia za elimu yenye manufaa kwa watu, ambayo hasa ndiyo elimu inayofaa kurithishwa katika jamii. Na Mtume[saw] alitufundisha kuwa miongoni mwa mirathi adhimu tunazopaswa kuziachia jamii zetu ni elimu yenye manufaa.
Anakariri katika hadithi ifuatayo akisema;

Idhaa maata bnu adamu inqatwa' 'amaluhu illa min thalaathati; swadaqatin jaariyatin au 'ilmin yuntafa' bihi au waladin swaalihin yad'u lahu.

Mwanadamu anapofariki matendo yake hukatika isipokuwa matatu: sadaka endelevu, au elimu yenye manufaa au mtoto mwema anayemwombea. (Sahih Muslim).

Katika hadithi hii tunafahamishwa juu ya umuhimu mkubwa wa kurithisha elimu yoyote yenye manufaa katika jamii. Hivyo kuisoma, kuiendelea na kuieneza elimu yoyote iwafaayo watu ni miongoni mwa sadaka kubwa katika Islam. Kama waahmadiyya, bila shaka tunayo dhima kubwa ya kuwa mstari wa mbele katika usomaji, uhamasishaji na uenezaji wa elimu zote zenye manufaa kwa watu.
Tunapaswa kufahamu kuwa kuelimika kwetu katika tasnia yoyote hakutakuwa na maana iwapo hatutatumia elimu yetu kwa ajili ya manufaa ya watu. Lengo letu kuu katika utafutaji wa elimu liwe ni kupata utambuzi juu ya uwepo wa Allah, ni kutokana na kuutambua vyema uwepo wa Allah ndipo tutapata uwezo wa kumhofu na kumwabudu.
Nadharia inathibitishwa kupitia aya ya Qur'ani Tukufu isemayo;

Innamaa yakhshallaaha min 'ibaadihil 'ulamaau.


Kwa hakika wamwogopao Allah miongoni mwa waja wake ni wale wenye elimu.
(35:29)

Hivyo kwa muumini kuwa na elimu kubwa juu ya fani fulani,

Itaendelea..... toleo lijalo Inshallah

MATUKIO KATIKA PICHA

Pichani ni Maulana Sheikh Shabani A. Shunda Sahib, akihutubia katika Darasa la malezi kwa Khuddam na Atfal Masjid Salaam jijini Dar es Salaam.



Pichani ni baadhi ya matukio katika semina ya Majlis Ansarullah huko Masasi - Mtwara, pamoja na kushiriki Jalsa ya Kanda



Jitafute Jitambue

Na.
Maulana Sheikh Shaban A. Shunda



Kwenye kila familia kuna mtu mmoja anabarikiwa ili kubadili historia ya familia, iwe kutoka katika umasikini kwenda utajiri, au iwe kutoka uduni kwenda umaarufu, udhalili kwenda kwenye heshima, au ufedhuli kwenda kwenye utakatifu.

Uteule huu sio kuwa atakuwa mtu mmoja kwenye familia kati ya kumi na wengine wawe wamenyimwa chochote bali kila mtu ni mteule sawa na wito wa uelekeo wa maisha yake katika kutimiza lengo lake. Katika familia mnaweza kutokea katika mila au familia ya kaliba na kazi Fulani lakini kati yenu kuna kila mtu ni mzuri katika kitu Fulani, basi ule uzuri katika kitu Fulani ndio wito au uteule ninaokwenda kuuzungumzia.

Kibiolojia kila mtoto hapa duniani huzaliwa akiwa na sifa za kipekee, maumbile tofauti yaliyojengeka na nguvu tofauti za kiakili na stamina. Huenda wewe mwenyewe ulihisi ukiwa mtoto, jinsi marafiki zako walivyokuwa tofauti na wewe.

Mara nyingi wazazi huwa wanatambua watoto na kuwakuza na wanajua yaliyomo ndani mwao toka wakiwa wadogo au kama wazazi ni watu wa mambo ya kiroho basi huwatambua hawa watoto toka hawajazaliwa kupita ndoto au maono mengine ya kiroho, imekuwa hivyo hapo kabla kwa Nabii Yusuf (as), Quran tukufu inatueleza uhusiano wake wa karibu na baba yake toka alipokuwa mdogo na ni jinsi gani Allah alimfanya kuwa nabii, bali mbali zaidi aliwaokoa ndugu zake kutoka kwenye taifa lenye uhaba wa chakula na kuwaleta katika nchi yenye neema ya Misri huku wakiwa na hadhi ya familia yenye utukufu na heshima. Na Hazrat Musa[as] tunaona ni jinsi gani Allah alimuandalia mazingira ya kubeba jukumu la kuwakomboa wana wa Israel katika utumwa wa miaka na miaka.

Kuna familia ambazo watu wote hawajiwezi kabisa na kuna nyingine ambazo labda wanajiweza kila mmoja katika nafasi yake, lakini yote kwa yote tunachozungumzia ni ule utofauti katika kujitafuta na kujipata na uwezo wa ufanisi katika kufanya jambo Fulani na kulitimiza kwa muonekano ambao mtu anasema huo ndio wa kuigwa.

Kwenye mahojiano Fulani bwana Shaquille O'Neal 'Big Shaq' aliyekuwa mchazaji wa kikapu nchini Marekani na sasa ni mmiliki wa biashara kubwa kubwa na makampuni zaidi ya hamsini aliulizwa na mtangazaji kuwa je anatumia vilevi, alijibu kuwa ndio anatumia vilevi japo kwa tahadhari sana kwani sio sawa kwake kuonekana amelewa na kuongea hovyo mbele za watu na akaeleza zaidi kuwa, huo ni muongozo aliopewa na baba yake alipomuambia kuwa ' kijana wewe ndio umechaguliwa katika familia kutuvusha na kubadilisha taswara yetu ya umasikini kuelekea utajiri hivyo basi haipaswi kufanya mambo ya hovyo'

Tatizo kubwa linalozungumzwa Afrika leo hii ni kwamba mfumo wetu wa elimu haumsaidii mtu kujikwamua kutoka katika changamoto zilizo tuzunguka, kwani haimjengi mtu kifkra kuwa mtengeneza suluhisho la matatizo yaliyopo au awe na uwezo wa kubadilisha changamoto kuwa fursa.

Na familia zetu hazina mlengo wa kumuangalia mtu shauku yake na kunyweshelezea na kuikuza ili ije iwe chanzo cha kujichumia kipato bali kuwa ufaulu wake baadaye. Unaweza kukuta huko vijijini kijana anaonyesha ubunifu wa ujenzi toka akiwa mdogo kwa kujenga vijumba vya udongo au ni mchoraji mzuri basi sawa na mazingira na uwezo wa familia Yule mtu ataishia kufanya kazi za kuajiriwa mashambani na atazeeka akiwa masikini ambaye hakuweza kufanya kazi ya wito wake.

Kwa zile familia zilizosogea kidogo unawezo ona mtoto sio mzuri katika masomo kabisa lakini kwa sababu mzazi ana uwezo wa kulipa ada basi ataendelea kumuhamisha shule kwa kuamini akisoma atafanikiwa, lakini kumbe huwenda kijana huyo anaweza kuwa mfugaji mzuri wa kuku na akajitengenezea kipato kikubwa kupitia wito wake wa ndani.

Mara nyingi binadamu pindi atakapojua jukumu fulani ni lake, basi hakuna kitakachomzuia kufanya jambo litakalomfanya kutimizia jukumu hilo kwa umakini kwa juhudi Fulani, kwa wale vijana wenzangu naweza kuwaambia kuwa mafanikio yoyote bila kujipa jukumu Fulani au kujipangia lengo huwezi kufanikiwa, mara nyingi wana masumbwi hupigana na wakishinda katika maneno yao ya shukurani huwa wana sema hii ni kwa ajili ya mama yangu au hii ni kwa ajili ya jambo Fulani, basi huo ndio uhalisia na msukumo wa yeye kufanya jambo hilo na ndio jukumu alilojibebesha na matokeo yake ndio huo ushindi. Kwa mfano Conor Anthony McGregor ni mwana masumbwi wa MMA (mixed martial artist) kutoka Ui-rish. Yeye ni Bingwa wa zamani wa Ultimate Fighting Championship (UFC) uzani wa Featherweight na Lightweight, na kuwa mpiganaji wa kwanza wa UFC kushikilia ubingwa wa UFC katika madaraja mawili ya uzani kwa wakati mmoja. Mafanikio yake haya yalianza kushuka alipobadili lengo la kwa nini yeye alichagua upiganaji, alipoanza alikuwa anasema kuwa anachotaka ni kumjengea mama yake nyumba nzuri, kuwa tajiri na kuhodhi baadhi ya mali kadhaa zitakazo mfanya asiwe masikini, hivyo basi ndani ya mda mfupi ilikuwa hivi kwamba ukikutana na Mc Gregor ulingoni ulikuwa huna chaguo ila kupigwa na akafikia malengo yake na kutimiza jukumu alilojipa kwa haraka mno. Lakini alipofikia mafanikio yake alishuka kwa haraka mno kwani alibadili hata mtindo wa upiganaji wake na pia aliingia kwenye boxing na kupigana pambano moja, aliporudi UFC aliambulia kushindwa mfululizo, vivyo kwa Usman Kamaru alikuwa mbaya mno kwenye ulingo kwa sababu Baba yake alikuwa amefungwa jela kwa kesi ya kubambikiwa na ilikuwa lengo lake ni kukusanya hela ili kumtoa gerezani hivyo ilikuwa akiingia ulingoni basi huchukui mda anakuweka chini, baba yake alivyotoka gereza Usman Kamaru sio Yule tena ameshapigwa mara mbili mfululizo mpaka sasa, kikubwa lengo na jukumu likisha badilika au kumalizwa basi mtu anakosa ufanisi. Na hawa wote niliwatolea mfano ni watu waliokuwa wamejipa lengo la kubadilisha historia za familia zao.

Huyu mtu mwenye lengo na jukumu akijitambua mapema, inabidi aishi kwa kujitolea mno kwani Mungu amemchagua kwa lengo maalum na inatakiwa alitimize. Mara nyingi binadamu akiwa na malengo makubwa basi husahau mambo ya kawaida, hapa juzi kati kulikuwa na picha ya Godoro limetandikwa sakafuni na ikaandikwa kwamba ndipo anapolala tajiri Elon Musk, na yeye alikuja kutoa maoni kuwa 'juzi iliyopita alilala kwenye kochi la rafiki yake sebuleni hivyo hamna geni' yeye utajiri alio nao tunaweza kudhani analala juu ya maji au mazingira mazuri zaidi ya hayo. Mteule yeyote hatakiwi kujiweka mbele yeye kwanza alenge kutimiza ndoto zake kwani maono huwekwa na Mungu kwenye fikira za mtu.

Mtume[saw] ameiishi mifano hii ya watu wenye malengo maalum vyema kuliko yeyote Yule Imesimuliwa na 'Aisha[ra] Godoro la kitanda la Mtume[saw]lilitengenezwa kwa kifuko cha ngozi kilichojazwa nyuzi za mawese. **(Bukhari)**

Naye aliitolea maelezo mazuri mno kuwa:

Kuna hadithi nyingine iliyosimuliwa na Umar bin Al-Khattab kwa Ibn Abbas (ra), akishiriki sehemu ya mwisho ya hadithi:

Pindi hadhrat Umari alipoenda kumtembelea alipomkuta amelala kwenye godoro hilo la majani ya mitende huku michoro yake ikiwa imechora mbavuni mwake alitoa machozi na kumuambia kuwa wafalme hawa wa kidunia walala kwenye magodoro ya gharama na wewe ukiwa mbora kuliko wao hali yako ni hii, alijibu kuwa wao wanaiishi duniani na sisi tunaishi akhera, sehemu nyingine alisema kuwa hii dunia ni kama msafiri aliyekaa chini ya mti na baadaye ataendelea na safari? **(Bukhari)**

Ndio maana waliofanikiwa au wenye ndoto za kufanikiwa hawapo kwenye makimbizano ya kujionyesha kuwa anaendesha gari ng'ali au nguo za bei kubwa n.k huwa wanachagua unyenyekevu na udhalili kwani kutimiza lengo na wito uliopo ndani yao ni muhimu kuliko kitu chochote.

Wengi huwa wateule katika jambo Fulani lakini maisha yetu yanakuwa ya kujihudumia wenyewe kiasi kwamba tunapoteza jukumu la kuzivusha familia zetu.

Kwenye mitandao nilikutana na stori ya mwekezaji Amos

Itaendelea…. Inshallah toleo lijalo

Kurani Tukufu kwenye Kilele cha Mlima Kilimanjaro

Kutoka uk. 12

hizo adhimu. Waliamua na kukubaliana kuwa, wachague vijana watalii wa kwanza watakao kwenda kupandisha Kurani Tukufu katika mlima Kilimanjaro. Chaguo la kwanza walielekeza mkoani Morogoro, ambako kuna mlima kama vile Mkuyuni. Wa kwanza kuchaguliwa alikuwa Mzee Mwishehe Juma na wa pili akachaguliwa Bw. Shwaibu Mohammed. Na hapa Dar es Salaam makao makuu ya Jumuiya ya Ahmadiyya Tanzania wakaona apatikane mmoja ambaye ni mimi Mwl. Athuman Ungele. Kikosi kikatimia msafara wa watu watatu. Tukaandaliwa Kurani Tukufu zenye tafsiri ya ligha mia moja. Tafsiri ya kwanza ni Kiswahili Kurani 10 lugha ya Kiingereza nakala 10, Kifaransa 10, Kitaliano 10, Kijerumani 10, Kirusi 10 na Kijapani 10 na nyinginezo nyingi za Afrika Mashariki bila kusahau Kiganda na Kijaruo. Na baadhi ya lugha zingine ambazo Kurani Tukufu Juzu chache. Tulianza safari 1989/03/20 kwa njia ya Treni hadi Moshi mjini. Tukapokelewa na wenyeji wetu wa Machame wakiongozwa na Mwl. Athuman Mgunya. Tulikaa siku mbili Machame tukaanza safari ya kuelekea Marangu. National park kuliko ofisi maalum kwa wapandaji wa mlima huo. Nakumbuka tulifika majira ya saa 3 asubuhi, tukapokelewa na wahusika. Tulifanya malipo ya kizalendo ya 21,000/= kwa sisi watalii wa ndani. Tukafanya malipo ya nguo maalum za kuvaa ukiwa njiani kupanda mlima huo. Fafanuzi ya juu ya nguo, mtalii anapaswa kuvaa kama ifatavyo, suruali 4, mashati 4, sweta 1, koti la mvua 1, soksi pea 4 ambazo zote huvaliwa kwa pamoja, na buti nzito. Kichwa kofia 4 za baridi pamoja na glavzi pea 2 bila kusahau fimbo (muongozo) ambayo ilikodishwa kwa 1,000/=. Gharama nyingine ni kumlipa kiongozi mzoefu 60,000/= kwa siku tatu. Msafara lazima wawepo wapagazi (porters) ambao watatubebea mizigo yetu pamoja na chakula. Mpaka hapo msafara wa kupanda mlima Kilimanjaro ulikuwa umekamilika. Tulipata changamoto moja, kuwapata viongozi wa msafara na wapagazi ilituchukua mda, walihofu kuwa waislam hawana pesa ya kuwalipa kulinganisha na wazungu. Hata hivyo tuliwapata na tukawalipa. Katika ofisi hii tuliacha nakala 2 za Kurani Tukufu, tafsiri ya Kiswahili pamoja na Kiingereza. Baada ya hapo msafara ulianza, ambao ulianza saa 5 asubuhi.

Waislam wa kwanza kupanda mlima Kilimanjaro kwa ajili ya kupandisha Kurani Tukufu za tafsiri mbalimbali ni pamoja na Marhun Mzee Mwishehe Juma, Mwl. Shwaibu Mohammed wote kutoka Mkuyuni Morogoro na Mwl. Athuman Ungele kutoka Dar es Salaam. Tukaunganishwa na kundi la watu sita kutoka Ujerumani. Tahadhali kubwa kutoka kwa kiongozi. Tahadhali ilitolewa kwetu kutoka kinywa cha kiongozi mzoefu wa mlima, ya kwamba tumpatie pesa tuliyokubaliana na kazi ya kuweka Kurani Tukufu zinazotakiwa ataweka yeye kwa sababu sisi sote hatutaweza kufika kilele cha kwanza kiitwacho Gilmans Point. Pia kuanzia sasa hapa tulipo geti la Marangu mda wowote mvua ya mawe (Barafu) kila siku unyesha. Ikikukuta njiani hujafika kituoni hutaweza kuachama midomo yako wala kuongea. Sisi sote tulimjibu *sisi wenyewe ni Wahmadiyya kiongozi ametutuma kuja kufanya hili, endapo tutakufa tupo tayari kwa ajili ya Mwenyezi Mungu*. Tukiwa njia hatujafika kituo cha kulala (Mandara Hallo) tuliwakuta wale wazungu wamekaa chini wakipumzika, sikufanya ajizi niliwapatia vipeperushi vinavyoelezea maana ya Islam kwa lugha yao.

Mmoja akajenga hoja akasema, Ee wewe unanitaka niwe Muislam, nikamjibu, hapa kusoma habari sio kuwa unatakiwa uwe Muislam, bali tu ujue Islam ni nini. Kwani sisi sote msingi wetu ni nabii Ibrahim. Akanielewa na akapokea. Baada ya saa 3 tulifika kituo cha kulala saa 8 mchana. Tulipofika kituo cha kwanza tulikabidhiwa kibanda cha Msonge wa mbao, ndani palikuwa pametandikwa magodoro matatu kwa ajili yetu. Tukachukua udhu (kutawadha) mmoja wetu akatoa adhana tukasali, maombi yetu ya kwanza ni juu ya msafara. Ee Mungu sisi hatuko katika safari ya anasa, tumekuja kufanya kazi yako, kwanini tushindwe kutimiza malengo yako, basi tunaomba utuwezeshe nia yetu na jina lako wasiolijua walijue kwa msafara huu. Mioyo yetu ilipata utulivu na kuendelea na ratiba zingine. Kituo hiki kina sehemu au meza maalumu ya kujisomea, nasi tukaweka vitabu vyetu ili wageni wajisomee. Vipindi vya ibada viliendelea kama kawaida hadi tarehe 24/03/1989 saa 3 asubuhi tulianza safari ya kuelekea kituo cha Horombo Hall tulitumia saa 3.

Tukiwa njiani kuelekea Horombo tulioneshwa kaburi la mtu aliyekufa kwa baridi kali akiwinda wanyama, alikuwa hana nguo maalum za kujikinga na mvua ya mawe. Tukafika Horombo salama. Hali ya hewa ilikuwa upepo mkali na baridi pia. Hapo ni siku ya pili mvua haijanyesha ambapo si kawaida ya mlima Kilimanjaro. Kila siku hunyesha mvua. Lile kundi la wajerumani lilikuwa tayari marafiri zetu. *You have any Medicine?* (Mnayo Dawa yoyote) nikamjibu we have not (Hatuna) akatupatia vidonge vya kuzuia kipanda uso, lakini hatukutumia. Mandhari ya eneo hili inapendeza sana, eneo lipo wazi kuonekana pale ulipotoka na unapokwenda. Moshi mjini kwaonekana vizuri mchana na usiku. Magharibi ya Horombo lile jiwe mlima halisi ulivyoinuka ni maajabu ya Muumba. Kaskazini mwa Horombo unaonekana mlima wa Mawenzi ambao hupandwa kwa kamba iliyoandaliwa rasmi. Kipindi chetu tumeikuta ndege ndogo imevutwa ikanaswa juu ya mlima huo wa Mawenzi. Watalii wa ki-Ahmadiyya tukaona hakuna sababu ya kuupitia mlima kwani hapakua na sehemu ya kuhifadhi kitabu chochote. Marafiki zetu walipitia tu bila kupanda mlima wa Mawenzi, nasi tulinyoosha kuelekea Kibo Halt. Hii ni siku ya tatu. Tulipokuwa njiani kuelekea Kibo Halt, hali ya hewa ni tofauti kabisa na sehemu mbili za nyuma, ndege warukao ni wachache, ni kama vile uwanja wa vita iliyopiganwa hivi karibuni. Tulianza kukanyaga kokoto nyeusi iliyoungua na moto wa Volcano toka juu ya mlima na kumwaga chini tutokako. Tulifika sehemu kuna jiwe kubwa limejiweka kama nyumba, sehemu hiyo watalii walikuwa wanalala saa 6 usiku kuamshwa na kuendelea safari ya kupanda mlima huo. Sehemu kuna jengo maalum la tofali lina milango na madirisha na jiko pia pamejengwa. Kutoka jiwe na kituo cha kulala cha zamani na jengo jipya Kibo Halt kama nusu kilometa hivi. Hapo katika jiwe ni lazima kupita nasi tuliweka Kurani zetu, ndipo tukaelekea Kibo Halt.

Tulifika Kibo Halt majira ya saa 6 mchana, na hali ya hewa ni nzito kweli kweli, pale tu kwenye jengo la kulala tulikuta Barafu imeota mlangoni. Tukaingia katika chumba ambacho kina vitanda na magodoro. Hali ya chakula katika kituo hiki, tukapewa mikate na chai ya rangi. Maziwa hayaruhusiwi ila biskuti na Coca-cola au Sprite, hali hiyo huufanya mwili kuwa mwepesi tayari kwa kupanda mlima. Katika chumba tulijisikia kama vile ndani ya friji, hapa ndipo tulivaa nguo zile nzito na kupanda kitandani. Saa 6 usiku kiongozi alikuja kutuamsha tutoke nje tayari kwa kuanza safari. Tuliitika wito sote tukatoka nje, kabla ya kuanza safari Marhun Mzee Mwishehe Juma akachuchumàa chini na kuanza kutapika. Kiongozi wa safari akawaita wapagazi ili kumrudisha ndani hadi asubuhi kurudishwa kituo cha chini ambacho ni Horombo. Tukabaki wawili Bw. Shwaibu Mohammed na mimi Mwl. Athuman Ungele pamoja na kiongozi wetu. Tulianza kupanda mlima saa 6:15 za usiku, wenzetu wajerumani walishatangulia. Mwendo ni wa guzi marchi au kukita miguu ili ubaridi usibaki mwilini utoke. Kutembea kwa kukita miguu inaweza kuwa mara kumi tu sawa na mita 5 lazima usimame upumzike mara tu unapata nguvu ya kuendelea na safari. Tindo ndiyo huo mpaka wa kufika nusu njia katikati ya mlima nako kuna pango la jiwe tukaweka Kurani yetu ya Kiingereza na vitabu vinginevyo. Hapo nusu ya njia tulifika saa9 usiku, bahati mle tunatembea hapajaota barafu, kiongozi alipata nafuu kutuongoza, vinginevyo kungekuwa na Barafu angefanya kazi ya ziada kuilima na kijembe kidogo ili mtalii apite kirahisi. Tuliendelea kukita miguu kutafuta kilele cha kwanza cha mlima kiitwacho Gilmans Point. Kwa msaada wa Allah akatuwezesha kufika kilele cha Gilmans Point alfajir saa 12:00 asubuhi. Tukionyeshwa jiji la Nairobi Kenya liko wazi. Nami nikaweka sahihi yangu pamoja na mwenzangu katika kitabu tulichokikuta hapo ndani ya boksi. Tukashuhudia bendera ya taifa ilivyowekwa na askari Alexander Nyirenda ikipepea kwa kasi. Nami nikaichukua Kurani Tukufu ya Kiswahili ya mwisho katika safari yetu, nikaiweka katika lile pango la jiwe lililotazama shimo kubwa la Barafu kwa wingi.

Kile kikosi cha wajerumani wote walifika hapa, baada ya kuweka sahihi walielekeza safari ngumu kuliko zote. Kutoka hapo ilipo bendera ili ufike Uhuru Peak itachukua muda wa saa 3 sawa

Endelea uk. 7

The First Muslim Newspaper in Swahili Language since 1936

Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania

Mapenzi ya Mungu

MAPENZI KWA WOTE BILA CHUKI KWA YEYOTE

HABARI UK> 5

Yesu aliongozwa na nani Nyikani?



HABARI UK> 10

Jitafute Jitambuwe

Kurani Tukufu kwenye Kilele cha Mlima Kilimanjaro



Na.
Mwl. Athuman Ungele Sahib

Ni kosa kubwa tena kubwa kweli kweli kuficha neema tulizoneemeshwa na Allah. Tumeombwa tuzidhilishe; Ahmaddyya ina sababu na wajibu wa kutoa shukurani kwa Allah hususan Jamati Ahmadyya Tanzania kwa kutumia Kuruani Tukufu katika kiswahili wazalendo waliamshwa kudai haki yao ya kuwa huru. Mapenzi ya Mungu likaanzishwa kurutubisha, kuenzi na kueneza Kiswahili. Jumuiya ikaandika vitabu katika Kiswahili, Sheria za kutunga mashairi na diwani ya Amri kikaamsha ari ya ushairi 1959 mkutano wa kwanza wa washairi ukafanyika ukumbi wa Masjid Salaam 1965 chama cha UKUTA Saidi Manoro Katibu Mkuu wa kwanza, kabla ya hapo 1960 mwafrika wa kwanza kuwa Meya wa jiji la Dar es Salaam Sheikh Kaluta Amri Abedi kwenye ubunifu usiseme. Jina Tanzania Mohamed Iqbal Dar, Hadubini Sheikh Jamil Rahman Rafiq, Bunge na Ikulu Sheikh Kaluta Amri Abedi. Al-Ustadh Khamis Sultan Wamwera mshairi akajibu utenzi wa Injili wa Mnyampala, Daktari bingwa wa saratani kutumia mionzi ya Nuklia mwanamke wa kwanza Tz Dr Tausi Kassim Maftah na leo tunaheshima kuwaletea simulizi kuhusu Ahmadiyya ilivyokuwa ya kwanza kuweka Kuruani Tukufu kileleni mwa Mlima mrefu kuliko yote barani Afrika simulizi inatolewa na aliyeshiriki Mwl. Athuman Ungele wa Kibiti Pwani.

Jumuiya ya waislam wa Ahmadiyya ilianzishwa kwa amri ya Allah na Sayyidna Ahmad[as] mnamo mwaka 1889. Sayyidna Ahmad[as] amefariki 1908. Baada ya kufariki kwa mwanzilishi wa Ahmadiyya, viongozi walioendeleza Jumuiya ya Ahmadiyya waliona waweke sherehe za umri wa miaka 100, endapo Jumuiya itatimiza muda huo. Hapa Tanzania Jumuiya ya Ahmadiyya ilikuwa chini ya ***Sheikh Waseem Ahmad Cheema*** na Katibu mkuu ***Mustafa Kapulilo***. Walifanya kikao rasmi ili watekeleze sherehe

UK. 11

FORTY SAYINGS OF THE HOLY PROPHET S.A.W.

By Sheikh Muhammad Munawwar H.A.
The book contains 40 short Sayings of the Holy Prophet s.a.w and ment for children

AHMADIYYA MUSLIM JAMAAT TANZANIA



HADITHI AROBAINI ZA MTUME MUHAMMAD s.a.w.

JUMUIYA YA WAISLAMU WA AHMADIYYA TANZANIA

Nakala hii itapatikana kwa Tsh. 1,000/=

Je, Wajua?

Je wajua kuwa ili ndege iweze kwenda mbele, hutoa upepo mbele na kuupuliza nyuma kwa kasi sana. Mithili ya puto lililopulizwa na kuachiwa bila ya kufungwa, huruka kwa sababu linatoa upepo kwa kasi. Meli pia hutoa maji mbele na kuyarudisha nyumakwa nguvu ili iweze kwenda mbele. Mpiga kasia katika mtumbwi nae hufanya kazi ya kutoa maji mbele na kuyasukuma nyuma ili mtumbwi

..... toleo lijalo Inshallah

Kwa Makala, Maoni, Ushauri; Tuandikie

mapenziyamungu36@gmail.com